

ARUSHA CO-OPERATIVE UNION LIMITED



Tel +255272546478
Email: info@acu.co.tz

P.O BOX 7073
Arusha
TANZANIA

In reply please quote:

22.10.2024

Ref No. AB.2/105/01/68

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUJITOlea (INTERNSHIP)

Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Arusha (ACU Ltd) kinatangaza nafasi mbili (2) za **AFISA KILIMO MSAIDIZI**.

KAZI ZA AFISA UGANI

1. Kuanzisha na kusimamia mashamba ya mfano.
2. Kukusanya takwimu mbalimbali za kilimo
3. Kusimamia Vyama vya Msingi katika kuandaa mashamba ya Chama.
4. Kutoa mafunzo kwa Wakulima kuhusu mbinu bora za kilimo.
5. Kutembelea Wakulima shambani.
6. Kushirikiana na watafiti wa kilimo na Wadau wengine wa kilimo katika kuongeza uzalishaji wa mazao bora ya kilimo.
7. Kusimamia ukusanyaji na tathmini ya takwimu za kilimo.
8. Kuandaa mpango wa mafunzo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo.
9. Kushirikiana na watafiti wa kilimo katika kutoa tahadhari kuhusu viashiria vya hatari vya magonjwa ya mazao.
10. Kutoa ushauri wa matumizi ya mbegu bora.
11. Kudhibiti visumbufu vya mazao.

12. Kuandaa na kuandika mpango kazi wa utekelezaji wa kilimo bora kwa Wakulima kwa kila msimu wa kilimo

SIFA ZA MWOMBAJI.

1. Kuajiriwa wahitimu wa Kidato cha nne (IV) au Sita (VI) wenyewe stashahada (Diploma) ya kilimo na mifugo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
2. Awe na uzoefu angalau mwaka mmoja kwenye shughuli za kilimo na mifugo.
3. Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika taarifa za kazi kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili.
4. Awe na uelewa wa kutumia kompyuta kwa programs za Ms Word, Excel, Power Point, Internet na E-mail.
5. Awe na uwezo wa kubuni na kuandika mipango mikakati inayohusu kilimo na ufugaji kwa faida za Wanachama husika.
6. Awe na uwezo wa kubuni na kuandika mipango ya utekelezaji inayohusu kilimo na wafugaji kwa faida za Wanachama husika.
7. Awe tayari kuhudhuria mafunzo mbalimbali yahusuyo kilimo ama ugani pale anapohitajika.

MASHARTI KWA MUOMBAJI WA NAFASI YA KUJITOLEA YA AFISA KILIMO

1. Muombaji awe ni raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 35
2. Muombaji aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Muombaji aambatanishe maelezo binafsi yanayo jitoshaleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini watatu wa kuaminika.
4. Maombi yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vya kidato cha Nne na cha sita, kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika, viambatanisho hivyo vibanwe sawasawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.
5. Muombaji awe tayari kufanya kazi Mkoa wa Arusha ama Mkoa wa Manyara Wilaya ya Kiteto kwenye shamba la ACU Ltd lililopo Songambele.
6. Picha moja ya "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma
7. Maombi yote yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa:-

**MENEJA MKUU,
CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA ARUSHA,
S.L.P. 7073
ARUSHA**

recruitment@acu.co.tz

au

info@acu.co.tz

Pia maombi yanaweza kuwasilishwa **kwa njia ya Email** ama katika ofisi za Chama Kikuu cha ACU Ltd zilizopo jengo la ACU mkabala na Maktaba ya Mkoa wa Arusha, Room Na.103. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **20/11/2024**.